**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**636** **TEHAMA**

**Muda: Saa 3 Hours** **Mwaka: 2019**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A**, na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka katika Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Ainisha misingi minne ya kuzingatia katika kutunga maswali ya kuoanisha.
2. Bainisha hatua nne za kufuata wakati mwanafunzi wa somo la TEHAMA anataka kufungua programu andishi kwa ajili ya kuchapa barua.
3. Eleza kwa kifupi hatua za kufuata unapofundisha mada ya usikivu katika somo la TEHAMA kwa kutumia kanda ya redio.
4. Bainisha mambo manne yanayotakiwa kufanywa na mwalimu wa somo la TEHAMA anapoandaa azimio la kazi.
5. Onesha kwa kifupi wanufaika wanne na jinsi wanavyoweza kunufaika kwa kutumia maktaba katika jamii.
6. Fafanua kwa kifupi faida nne za kusafirisha vifurushi kupitia Shirika la Posta.
7. Eleza kwa kifupi umuhimu wa zana nne zinazotakiwa kutumika katika kufundishia mada ya huduma za Posta.
8. Onesha maeneo manne maalumu ambayo alama za kuashiria hatari hutumika.
9. Changanua faida nne za kuwatumia wanafunzi katika kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia somo la TEHAMA.
10. Ainisha sifa nne za malengo mahususi katika andalio la somo la TEHAMA.

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **Manne** katika sehemu hii.

11. Eleza umuhimu wa kutumia vifaa vya TEHAMA wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.
12. Eleza faida zipatikanazo katika ufundishaji wa somo la TEHAMA kwa vitendo.
13. Elezea vikwazo vitano vinavyolifanya somo la TEHAMA kushindwa kufundishwa kwa ufanisi katika shule za msingi nchini Tanzania.
14. Fafanua hoja tano juu ya umuhimu wa kutoa mitihani kwa wanafunzi katika somo la TEHAMA.
15. Eleza mambo yanayoweza kuathiri uwasilishaji wa habari iliyosemwa.
16. Toa hoja tano kuthibitisha kauli hii: "Kufanya majaribio ya zana kabla ya kuitumia darasani ni jambo la muhimu sana."


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org